

TALIRI yaja na utafiti wa tija kwa wafugaji

Na Mbaraka Kambona

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), imesema imejipanga ku-hakikisha inafanya utafiti wa kutosha ili matokeo yake yatumiwe na wafugaji moja kwa moja badala ya utafiti wa mambo ya sayansi tu.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Prof. Erick Komba, baada ya kumaliza kikao kazi cha kujadili mkataba wa utend-

aji kazi wa taasisi hiyo kili-chofanyika jijini Dodoma Juza.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kufanya utafiti na kueneza teknolojia ya utafiti huo ili kuendelea kuboresha tasnia ya mifugo.

"Tumejikita katika kufanya utafiti wa malisho na mifugo ili kuwafanya wafugaji waweze kusuga kwa tija na kunufaika na mifugo yao," alisema Prof. Komba.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha uongozi wake,

atahakikisha utafiti wana-zozifanya zinaendelea ku-wanufaisha wafugaji na taifa kwa ujumla.

Aidha, Prof. Komba aliwhimiza watendaji wa taasisi hiyo kufanyakazi kwa wledi, na kwa bidii ili waweze kuzalisha utafiti wa kutosha na kuusambaza kwa wafugaji waweze kuutumia na kuiongezea kipato.

"Tangu nimeteuliwa kuongoza taasisi hii nina miezi miwili sasa, lakini milango yangu ni kuhakikisha

ninashirikiana kikamilifu na watafiti wenzangu kufanya tafti zitakazoleta matokeo yatakayowasaidia wafugaji kupata tija na sio utafiti kwa ajili ya sayansi tu," alisefanua Prof. Komba.

Naye Mwenyekiti wa Bodii ya TALIRI, Prof. Sebastian Chenyambuga, alisema wajibu wa taasisi hiyo ni kufanya utafiti, hivyo aliwataka watumishi wahakikishe wanajipanga vizuri illi kazi zao ziwe na manusaa kwa wananchi hususan wafugaji.

NIPASHI UK. 9 , JUNI 18, 2021